# Orodha Kaguzi ya Usajili wa Mara Mbili ya HACC

## Mchakato wa Usajili

- Ratibu mkutano na mshauri wako ili mjadili ikiwa usajili wa mara mbili unakufaa.
- Kamilisha kujaza fomu ya Ombi la Usajili wa Mara Mbili wa School District of Lancaster na upate idhini ya mshauri wako na usimamizi wa kampasi. Unaweza kupata fomu ya ombi kutoka College and Career Center (JP 147, East A126) au ofisi ya ushaui.
- Inapoidhinishwa, tembelea College and Career Center ili mjadili hatua zinazofuata.
- Kamilisha ombi la HACC. Maombi yanapatikana mtandaoni au kwenye College and Career Center. Fahamu kuwa maombi yanahitaji sahihi za mwanafunzi *na* mzazi/mlezi.
- Omba nakala ya hati yako itumwe kwa HACC. Lazima uombe hii kutoka kwa mshauri mwenyewe au kupitia Xello.
- College and Career Center itatuma ombi lako kwa njia ya barua pepe kwa HACC Admissions Counselor, Chala Thomas .cmthomas@hacc.edu
- Baada ya ombi kuchakatwa na HACC, utapokea barua pepe ya thibitisho kwenye barua pepe ya binafsi uliyoweka kwenye ombi, ikifuatiwa na barua pepe ya pili kutoka HACC ikitoa maelezo ya kuingia ya "myHACC'.
- Unapopokea barua pepe hizi, lazima uratibu jaribio la kusoma, kuandika na hisabati **AU** utoe alama zako za SAT au ACT. Toa alama zako za SAT ikiwa ulipata alama 480 au juu katika Evidence-based Reading/Writing na 550 na juu katika hisabati. Ikiwa ulipata zaidi ya alama hizi, huhitaji kufanya jaribio la kuwekwa kwenye darasa.
- Fanya jaribio la kuwekwa kwenye darasa. Lazima uwe na kitambulisho cha picha ili ujaribu. Jaribio linapatikana nyakati zifuatazo kwenye jengo Kuu katika Kampasi ya Lancaster (hakuna miadi inayohitajika). Pitia tu Welcome Center ili utie sahihi:

  **Jumatatu kati ya saa 9 asubuhi na 2 alasiri**
  **Jumanne, Jumatano na Alhamisi, kati ya saa 9 asubuhi na saa 6**
  **jioni Ijumaa kati ya saa 9 asubuhi na 2 alasiri**
- Baada ya jaribio la kuwekwa kwenye darasa, kamilisha kujaza fomu ya usajili wa kozi ili uchague darasa unalotaka la muhula. Wanafunzi wanapaswa kuzungumza na Mshauri wa Usajili wa HACC baada ya kufanya jaribio au kuratibu wakati ili kupanga madarasa. Unaweza kuwasiliana na HACC Admissions Counselor Chala Thomas kwa cmthomas@hacc.edu.

## Baada ya Usajili

- Chukua kitambulisho chako cha HACC kwenye Welcome Center
- Chukua vocha yako ya kitabu cha mazoezi kwenye Welcome Center. Fahamu kwamba unaweza tu kununua bidhaa zinazohitajika kwa darasa. Utatozwa kwa gharama zozote za ziada.
- Chukua vitabu kwenye HACC Bookstore: Utahitaji kitambulisho cha HACC, Vocha na ratiba ya sasa ya HACC ili upate vitabu vyako.

- Inayopendekezwa: Hudhuria maelekezo ya usajili wa mara mbili. Hii inaweza kuwa kwenye kampasi katika McCaskey au HACC-Lancaster.
- Tunakutakia muhula bora!

**Inaendelea Muhula Mzima**

- Endelea kuwasiliana na College and Career Center – (East A126 au JP 147)